

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TAREHE: 04/02/2025

## TAARIFA KWA UMMA

Katika kusogeza na kurahisisha utoaji na upokeaji wa huduma kwa Wananchi, kuanzia Februari 04, 2025 Manispaa ya Kinondoni imeanzisha Kanda zitakazoanza kutoa huduma kwa Wananchi katika maeneo yote. Huduma zitakazotolewa ni Pamoja na upatikanaji wa huduma za malipo ya tozo mbalimbali kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri. Aidha, Ofisi hizi za Kanda zitakuwa wazi kwa siku za mwisho wa Mwezi ili kuwarahisishia Wananchi kuendelea kupata huduma.

Huduma zitakazo patikana katika Ofisi hizi za Kanda ni pamoja na ulipiaji wa:

- Kodi ya Huduma (Service Levy); Leseni za Biashara, Upimaji afya
- Hotel Levy; Ushuru wa Taka; Vibali vya Ujenzi; Madini Ujenzi
- Maeneo ya Wazi; Leseni za Vileo; Leseni za Uvuvi
- Leseni za Vyombo vya Uvuvi; Tozo za Parking za Magari
- Kodi za mabango; Vibali vya kupiga muziki na Kodi za Majengo.

Ofisi hizi za Kanda ni kama ifuatavyo:

1. **Kanda ya Magomeni - Makao Makuu:** itahusika na Kata za Magomeni; Ndugumbi; Mwananyamala; Kinondoni; Hananasifu; Kigogo na Tandale.
2. **Kanda ya Kibo Complex (jengo la Kibo Complex):** Itahusika na Kata za Kunduchi; Mbezi Juu na Kawe
3. **Kanda ya Bunju (jengo la Ofisi ya Mtendaji Kata ya Bunju):** itahusika na Kata za Bunju; Mbweni na Mabwepande.
4. **Kanda ya Namanga (Ofisi ya Manispaa ya kulipia tozo-Namanga):** itahusika na Kata ya Msasani
5. **Kanda ya Mwenge (Ofisi za Manispaa za kulipia tozo):** itahusika na Kata za Kijitonyama; Makongo na Makumbusho
6. **Kanda ya Wazo (Ofisi ya Mtendaji Kata ya Wazo-Salasala):** itahusika na Kata za Wazo na Kunduchi

**7. Kanda ya Mikocheni (Ofisi ya Kulipia tozo): itahusika na Kata ya Mikocheni.**

Hivyo, tunatoa wito kwa Wananchi wote waliopo Manispaa ya Kinondoni kufika katika Ofisi ya Kanda iliyopo karibu nawe ili uweze kuhudumiwa kwa ukaribu na uharaka zaidi.

Imetolewa na



Imeandaliwa na;

Aquilinus Shiduki

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Manispaa ya Kinondoni.